**Learning by Ear – Elimu na Kazi**

**Masomo ya chuo Kikuu - Hadithi ya Malaika / Episode 04**

**Mwandishi: Njoki C. Muhoho**

**Mhariri: Maja Dreyer**

**Tafsiri: Eric Ponda**

Wahusika:

| | |
|---|---|
| Mtangazaji | - Mwanamume |
| Malaika | - Msichana wa miaka19 |
| Bw Baraza | - Mfanyi biashara mwanamume miaka 55. |
| Bi Grace | - Miaka 52 |
| Shangazi Tizo | - Miaka 64 |
| Mzee Nathan | - Babake Malaika miaka 60 |
| Mama Rose | - Mamake Malaika miaka 45. |

**INTRO**

**MUZIKI**

**MTANGAZAJI** HUJAMBO NA KARIBU KA MAKALA YA NNE YA MFULULIZO WA VIPINDI VYETU VYA “LEARNING BY EAR” MADA IKIWA NI ELIMU NA KAZI.

KATIKA KIPINDI CHETU CHA MWISHO, MALAIKA AMEGUNDUA CHANGAMOTO MAISHANI KATIKA CHUO KIKUU NA VILE

VILE MANUFAA YAKE. AMEPATA VIDOKEZO TU KUHUSU NAMNA YA KUJUMUDU KIMASOMO CHUONI, KUFANYA KAZI WAKATI WA MAPUMZIKO NA PIA WASAA WA KUFURAHISHA NAFSI YAKE. PIA AMEGUNDUA KWAMBA KUNA MENGI YA KUJIFUNZO MBALI NA MASOMO DARASANI. SASA AMERUDI NYUMBANI KWA LIKIZO YA KWANZA KABISA TANGU AJIUNGE NA CHUO KIKUU. JE ANAYACHUKULIAJE MAISHA YA KIJIJINI, BADO VILE VILE AU AMEBADILIKA?

***<u>SCENE 1: NYUMBANI KWA MZEE NATHAN</u>***.

**Sauti za shambani, mlio wa Ngombe, Mbuzi na ndege wakiimba**.

| | | |
|---|---|---|
| 01. | MAMA ROSE | ***(akiita kutoka mbali)*** Malaika!… Malaika… Njoo upesi. |
| 02. | MALAIKA | ***(akichakura makaratasi, nakunungunika)*** Ahhh,…. tena Mama ***(kwa sauti )*** Nasoma Mama!. |
| 03. | MAMA ROSE | ***(akikaribia )***Malaika, nitakuita mara ngapi, njoo haraka unisaidie kuzirejesha ng´ombe zizini. |
| 04. | MALAIKA | Samahani mama… nilikuwa nasoma! |

05. MAMA ROSE Lakini si hiyo ndio kazi unayofanya huko chuoni siku zote! Kwa hivyo hutatusaidia kwa kuwa unasoma!

06. MALAIKA Samahani mama. Kwanini nisiwasaidie, ni kwa vile….

07. MAMA ROSE ***(akimkatiza )*** Toka nje haraka wewe msichana! Bado wewe ni binti yetu na una wajibu wa kutekeleza hapa nyumbani… toka haraka!

08. MALAIKA Sawa mama, natoka... lakini nakuomba unipe muda wa kusoma baadaye!

*09.* MAMA ROSE ***(akinungunika).*** Mimi sielewi ni elimu gani hii ya sasa? Mtu anasoma mpaka anajisahau kula… kufanya kazi… na hata kutangamana……! ***(sauti ikitoweka)***

**Muziki**

**<u>SCENE 2: SHAMBANI</u>**

**SFX: Sauti za shambani, mlio wa ngombe, mbuzi na ndege wakiimba.**

10. MZEE NATHAN Hebu tazama Malaika jinsi mazao yetu yalivyoathirika na kunyauka! Ni lazima tushirikiane kufanya kazi kwa bidii shambani ili

tuzalishe chakula cha kutosheleza familia yetu…na unapasa utusaidie!

11. MALAIKA Baba…! unakosea.., sivyo hivyo..!

12. MZEE NATHAN Ehh msichana, tangu lini ukawa mwalimu wangu kunitia chuoni? Watoto wa siku hizi… wewe ….!

13. MALAIKA ***(akimkatiza)*** Baba ulinipeleka chuo kikuu kusoma, na sasa haya ndio matunda yake eti, tuseme ndio unaanza kuvuna matunda hayo sasa! Hili shamba umekuwa ukipanda miaka nenda miaka rudi. Unapasa kuligawanya kama mara tatu hivi. Sehemu moja uweke ng’ombe, nyingine upande maharagwe, nyingine mahindi na kadhalika, kisha msimu ujao ubadilishe!

14. MZEE NATHAN Kwani mimea imekuwa kipepeo… kuruka kutoka boma moja hadi jingine.

15. MALAIKA Kwa hilo, yawezekana baba. Wakati kipepeo anaporuka kutoka ua moja hadi jingine, hubeba chavua na vitu vingine vya manufaa kwa ua jingine, huku kipepeo hicho pia kikinufaika na maua hayo. Ni sawa na shughuli za kilimo baba. Baadhi ya mimea hutumia aina fulani ya rotuba ardhini ilhali mimea mingine ina mahitaji tofauti ya rotuba katika ardhi hiyo. Kwa hivyo,

kwa kuzingatia kilimo cha mzunguko, kila mumea utapata mahitaji yake ardhini huku ardhi nayo ikiendelea kuhifadhi rotuba yake na kuzalisha mazao mazuri.

16. MZEE *NATHAN* ***(akisafisha koo)*** Unajua nini wewe? Una maana uzee si hekima siku hizi!

17. MTANGAZAJI Malaika sasa amekuwa mshauri wa babake. Pia alimuahidi mwalimu Grace kwamba atamsaidia na kazi zake shuleni, ili kulipa mkopo aliopewa na mwalimu huyo. Siku inayofuatia Malaika anazuru shule alikosomea,lakini wakati huu akiwa na jukumu tofauti…..

***SCENE 3: KATIKA SHULE YAKE YA MSINGI ALIKOSOMEA*.**

**SFX: SAUTI ZA WATOTO WAKICHEZA SHULENI, KENGELE YA SHULE INALIA, KISHA KIMYA….**

BI. GRACE Niliahidi kumshtukiza leo. Sasa Malaika ambaye ni mwanafunzi wetu wa zamani mwaka uliopita ametutembelea. Karibu Malaika, na tunakushukuru kwa kututembelea.!

WANAFUNZI Wanapiga makofi na kumshangilia.

MALAIKA Hamjumbo wanafunzi. Nimefurahi kuwatembelea tena hapa nyumbani. Nataka tu kuwahimiza msome kwa bidii na bila shaka mtafaulu. Pia nyinyi mnaweza kufanya vyema na kupita mitihani yenu kisha kujiunga na chuo kikuu kama mimi. Hata hivyo maisha ya chuo kikuu si rahisi, kazi ni nyingi ingawa kuna raha zake. Pia kule utapata marafiki wengi na kujifunza mambo mapya kuhusu maisha. Mimi ni kama nyinyi tu, nimezaliwa hapa, na kusomea katika shule hii ya msingi. Kwa hivyo msijihisi kwamba eti mnatoka kijiji maskini, shule duni au kwa sababu wewe ni msichana huwezi kufaulu! Yote yategemea wewe mwenyewe na bidii yake na jinsi utakavyojichukulia. Uwezo mnao, ila tu namna ya kuutumia...

Wanafunzi. **Wakipiga makofi na kumshangilia/Mbinja**

BI GRACE: Huo ulikuwa ushauri na ujumbe mzuri sana Malaika…umenifurahisha! Sasa twende ofisini mwangu… ***(kimya kidogo wanapotembea kuelekea ofisini).*** Malaika kwanini waonekana mnyonge?

MALAIKA: Hali ni ngumu mwalimu Grace, kazi nyingi na watu wana matarajio makubwa kutoka kwangu.

BI GRACE : ***(akikubaliana naye)*** Ukitaka kumla ng'ombe utaanzia wapi?

MALAIKA: Eti Nini?

Bi GRACE Sikiliza, ukitaka kumla ng'ombe, utaanzia wapi.. au utamla tu mara moja?

MALAIKA: La hasha!

Bi. GRACE Ninamaanisha hivi. Bila shaka utamla hatua kwa hatua sivyo? Najua sasa umeanza kuogopa usijeanguka mtihani wako.

MALAIKA ***(kwa huzuni*** ) Ndio!

BI GRACE Hebu nisikize kwa makini, kuanzia leo, nataka ufanye mambo yako hatua kwa hatua, huwezi kufanya kila kitu kwa wakati mmoja. Kwanza ujue unachotaka maishani, kisha uelekeze juhudi na fikra zako kufanikisha malengo hayo.

MALAIKA Asante Mwalimu Grace kwa ushauri wako. ***(kimya)*** Ehh… nafikiria tuanzishe masomo ya komputa hapa. Tunaweza kununua mashini moja ya kompyuta na kisha nianze kuwafunza wanafunzi masomo ya ICT.

Bi. GRACE: IEE CEE … nini?

MALAIKA *(**acheka**)* Kwa sasa hivi kuna mabadiliko makubwa ya teknolojia kote ulimwenguni na wanafunzi wanapaswa kujifunza hayo.. (***Sauti ikitoweka….*** )

***Muziki wa chini kwa chini.***

**Mtangazaji:** Malaika sasa anajaribu kusaidia kijiji chake kutokana na yale anayojifunza chuoni. Lakini licha ya elimu yake ya chuo kikuu. Wazazi wake bado hawajabadili nia na msimamo wa kumuoza binti yao. Na nyumbani mgeni anamsubiri Malaika.

**SCENE 4: NYUMBANI KWA MZEE NATHAN.**

**SFX: Ndege wakiimba, mbuzi wakilia na sauti na moto ukiwaka.**

MZEE NATHAN *(**Akisafisha koo**)*

MAMA ROSE: Funga domo lako haraka Malaika, la sivyo nzi watajenga makao…

MALAIKA: Siamini, bado munadhani natakiwa kuolewa!

MZEE NATHAN Malaika, wajua bwana Baraza anasifika sana hapa kijijini kwetu. Ni mtu tajiri na anataka kukuposa.

MALAIKA. Baba!

Bw BARAZA: Ehhe nataka uwe mke wangu wa mwisho…..chenza.. …kipusa, ua langu… wajua mke wa mwisho huishia kupendwa sana!

MALAIKA Mimi nataka shamba nitakalokuza chenza zangu, maua mengi mazuri na mazao mengineyo, lakini sio mimi kufanywa ua, yaani kuolewa!

MAMA ROSE Chunga domo lako! Bwana Baraza ni mtu mkarimu atakulipia karo ya chuo kikuu. Bado hatuna pesa za kulipa karo yako muhula ujao, na kama ujuavyo bado tunadaiwa na mwalimu

MZEE NATHAN Tayari nimekubali posa ya bwana Baraza. Na hii ni kwa manufaa yetu sisi sote. Wewe uendelee na masomo yako, sisi tupate mahari na Baraza apate mke atakayemsaidia maishani…

MALAIKA *(**akisisitiza msimamo wake**)* Bw Baraza, si unafanya biashara mjini, sivyo? Kwa nini usiniruhusu nisikusaidie na shughuli zako za kibiashara, unilipe nusu ya mshahara wangu na kiasi kinachosalia uwape wazazi wangu. Kwa kufanya hivyo, nitakuwa nakusaidia kuimarisha biashara yako, huku unanisaidia pamoja na

wazazi wangu! Hii itamnufaisha kila mmoja wetu … ama sivyo baba?

**MUZIKI**

**<u>OUTRO</u>**

**MTANGAZAJI** MALAIKA SASA NI MWANAFUNZI ANAYESHIKA MAMBO HARAKA, LAKINI BADO ANAJIKUTA KATIKA NJIA PANDA BAINA YA MAISHA YA KIJIJINI NA YALE YA JIJI, MATARAJIO YAKE YA CHUO KIKUU NA YALE YA KIJAMII HIVI KARIBUNI ATAREJEA CHUONI KUENDELEA NA MASOMO YAKE. JE ATAJIMUDU VIPI?.

Ungana nasi tena kwa kipindi kijacho cha 'Learning by Ear' kuhusu Kazi na elimu ya Chuo kikuu.Unaweza pia kujifunza mengi kuhusu vipindi vyetu vya Learning By Ear' kupitia mtandao wetu www.dw-world.de/lbe. Hadi wakati mwengine Kwaheri